



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

MAAMUZI YA KAMATI YA MAADILI TAIFA

Ninapenda kuutaarifu umma kuwa leo tarehe 17/10/2015, Kamati ya Maadili ya Kitaifa imekutana na kusikiliza na kuamua malalamiko kutoka Tume ya Taifa ambayo ni mhusika wa Maadili dhidi ya Ndugu Duni Haji wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo ambacho pia ni mhusika wa Maadili.

Mlalamikiwa wa uvunjaji wa Maadili ni mgombea mwenza wa CHADEMA, **Ndugu Duni Haji**. Malalamiko yanahusu kauli zilizotolewa na mgombea huyo kuwa Tume imeongeza vituo hewa zaidi ya 20,000 vya kupigia kura. Hivyo Ndugu Duni Haji aliandikiwa barua na Katibu wa Kamati ya Maadili kujulishwa malalamiko hayo, na alipewa nakala ya barua ya malalamiko na ushahidi wa maandishi pamoja na video (na sauti yake Ndugu Duni Haji) katika uwanja wa Furahisha, Jijini Mwanza.

CHADEMA, pamoja na mjumbe wa Kamati (John Mallya) hawakujibu barua wala kufika kwenye kikao cha kamati japo wanakiri kupokea barua na kupigiwa simu. Kamati ilikutana muda wa saa 4.00 asubuhi na waliwasubiri Ndugu Duni Haji pamoja na Mjumbe wa Kamati kutoka CHADEMA, mpaka saa 5.00 asubuhi bila kufika.

Kamati iliamua kuanza kikao na kujadili malalamiko hayo. Kwa kuwa CHADEMA, waliidharau Kamati, Kamati ya Maadili imefikia maamuzi ya kumwadhibu Ndugu Duni Haji kwa kuzingatia Kifungu cha 5.10 (b) na (c) cha

Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2015, ambayo CHADEMA waliyasaini kama Vyama vingine. Adhabu hiyo ni;

- (a) Kamati inatoa onyo ka Ndugu Duni Haji kutorudia kutoa taarifa zisizo sahihi kwa Umma.
- (b) Kamati inatangaza Jina la Ndugu Duni Haji Mgombea Mwenza wa CHADEMA kuwa amekiuka Maadili ya Uchaguzi kwa kuudanganya Umma kuwa Tume imeongeza vituo hewa zaidi ya 20,000 vya kupigia kura.

Imetolewa na

Jaji Mkuu (Mst. Z) Hamid M. Hamid
MWENYEKITI WA KAMATIYA MAADILI KITAIFA
Leo tarehe 17/10/2015